

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA



MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI - FEBRUARI 2025 SANAA NA MICHEZO – DARASA LA NNE

Muda: Saa1:30

Mwaka: 2025

SEHEMUA


1. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uiandike katika mabano uliyopewa.

i. Miondoko ya mwili katika uigizaji husaidia hadhira kuelewa uhusika na ujumbe wa mwigizaji. Ipi kati ya zifuatazo **siyo** moja ya miondoko hiyo?

- A. Kusimama wima B. Kuangalia chini
C. Kukunja mikono kifuani D. Kukimbia na kurukaruka juu []

ii. Mwigizaji anaweza kutumiakupata video au picha za anayemwigiza ili kuchunguza kwa umakini miondoko yake.

- A. VITABU B. TEHAMA C. MKAO D. MALEBA []

iii.  Picha hii ni mfano wa mwigizaji anayefanya mazoezi ya nini?

- A. Kucheka B. Kuongea C. Kulia D. Kucheza []

iv. Ipi ni faida ya ufunguaji mzuri wa mdomo wakati wa uimbaji?

- A. Kutamka maneno kwa wakati sahihi B. Kutamka kwa usahihi irabu na konsonanti
C. Kudhibiti mtiririko wa hewa D. Kujua maana ya neno []

v. Uimbaji unaosindikizwa na ala za muziki ni sanaa yenye ujuzi na ufundi. Kipi unadhani ni muhimu kwa waimbaji na wapiga ala za muziki wanapaswa kukifanya?

- A. Kufanya mazoezi ya pamoja mara kwa mara B. Kuacha kutumia ala za muziki
C. Wote kupiga ala za muziki D. Kufanya mazoezi usiku ili kupata utulivu []

vi. Je, mtu anayeigiza anajulikana kwa jina gani kulingana na kazi yake?

- A. Hadhira B. Mhadhiri C. Mwanamitindo D. Muigizaji []

vii. Moja ya kanuni katika uimbaji wa sauti mbili ni ipi kati ya zifuatazo?

- A. Waimbaji wa sauti zote wanapaswa kuwa pamoja
B. Waimbaji wa sauti ya kwanza wakae pamoja na wa sauti ya pili wakae pamoja
C. Waimbaji wote wa sauti ya kwanza wakae chini
D. Waimbaji wote wa sauti ya pili wasimame []

viii. Ipi kati ya zifuatazo si miongoni mwa ala za muziki?

- A. Marimba B. Filimbi C. Ngoma D. Toni []

ix. Vifuatavyo ni baadhi ya vifaa ambavyo hutumika katika uchoraji isipokuwa?

- A. Karatasi B. Kibanio C. Penseli D. Chupa []

x. Kipi kati ya vifani vifuatavyo kinaweza kufinyangwa kwa njia pindi?

- A. Chungu B. Piramidi C. Mchemraba D. Mchemstatili []

JINA LA MTAHINIWA: SHULE:
MKOA: WILAYA:

SEHEMU B

2. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha uliandike katika nafasi wazi.

penseli,	ufutio,	kumbukumbu za hisia,	hadhira,	fanani
----------	---------	----------------------	----------	--------

- Ugizaji hufanyika mbele ya
- Kifaa kinachotumika kufuta makosa katika shughuli za uchoraji.
- Kifaa kinachotumia kuchora maumbo
- husaidia kuamsha hisia zinazohitajika wakati wa kuigiza.


SEHEMU C

3. Oanisha vifungu A na B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya majibu.

ORODHA A	MAJIBU	ORODHA B
i. Namna mtu anavyoweka mwili wake wakati amesimama, amekaa au anatembea		A. Maleba
ii. Kifaa kinachoongeza mafuta au kasi ya gari		B. Mkao
iii. Mavazi ya wasanii wakiwa kwenye onesho		C. TEHAMA
iv. Kuwasiliana kwa kutumia viungo vya mwili bila sauti		D. Kichapuzi mafuta
v. Teknolojia ya habari na mawasiliano		E. Lugha ya vitendo
		F. Kifani

SEHEMU D

4. Tazama picha hiyo kisha ujibu maswali.



- Mchoraji amechora kitu gani?
- Hii ni aina gani ya picha?
- Ni penseli ya aina gani inafaa kuchorea picha hiyo?

SEHEMU E

5. Chunguza kwa makini picha zifuatazo kisha ujibu maswali.



- Taja kifaa kilichotengenezwa kwa kutumia ngozi ya mnyama
- Vifaa hivi hujulikana kama
- Andika jina la kifaa kati ya hivyo ambacho hutoa sauti kwa kupulizwa.